# JARIDA LA USHIRIKA

TANZANIA CO-OPERATIVE DEVELOPMENT COMMISSION
TCDC
Together We Build Our Economy

ISSN 2714 - 2175 | Toleo Na. 16 | Septemba - Desemba, 2024







*Ushirika - Pamoja Tujenge Uchumi*

# YALIYOMO


1. KUTOKAKWAMRAJIS....................................................................................................1

2. RAIS DKT. SAMIA AUNGA MKONO MAGEUZI KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA..................................2-3

3. NUKUU ZA VIONGOZI KUHUSU USHIRIKA.....................................................................................4

4. SACCOS TUMIENI MIFUMO YA KIDIGITALI - NAIBU WAZIRI SILINDE.............................................5-6

5. TANECU YAANZA SAFARI YA KUWA NA USHIRIKA IMARA KWA KUJENGA KIWANDA.........................7-8

6. RC HOMERA AWATAKA WANANCHI KUTUMIA HUDUMA RASMI ZA KIFEDHA.....................................8-9

7. JEWAJUA?...............................................................................................................................10

8. TCDC NA CBE ZADHAMIRIA KUTOA MAFUNZO YA KUENDESHA USHIRIKA KIBIASHARA......................11

9. UJUE MWONGOZO WA UWEKEZAJI KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA................................................12

10. USHIRIKAWAGHOMACOSUNAVYONEEMESHAMAISHAWILAYANI SERENGETI...............................13-14

11. USHIRIKI WA TANZANIA KATIKA MKUTANO MKUU WA SHIRIKISHO LA VYAMA VYA USHIRIKA DUNIANI (ICA) 2024.....................................................................................................................15

12. IMARISHENI MIFUMO KUZUIA UPOTEVU WA FEDHA KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA - NAIBU KATIBU MKUU, KILIMO.....................................................................................................16-17

13. MRAJIS ATEUA WAJUMBE WA BODI YA MPITO YA SHIRIKISHO LA VYAMA VYA USHIRIKA TANZANIA (TFC).........................................................................................................................18

14. TCDC KUENDELEA KUWAJENGEA UWEZO WATUMISHI....................................................................19

15. VYAMA MBALIMBALI VYA USHIRIKA VYAKABIDHI BIDHAA MBALIMBALI KWA JAMII........................20

16. VIBONZO VYA USHIRIKA...........................................................................................................21

17. MATANGAZO MBALIMBALI.........................................................................................................22

# KUTOKA KWA MRAJIS



*Dkt. Benson O,Ndiege*
*Mrajis na Mtendaji Mkuu wa TCDC*

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) inakuletea Jarida la Ushirika Na. 16 kuhusu habari, matukio, matangazo pamoja na masuala mbalimbali ya Ushirika katika kipindi cha Septemba - Desemba 2024.

Katika kipindi hiki Tume ilipata fursa ya Kipekee pamoja na Watendaji wengine wa Wizara ya Kilimo kukutana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na kufanya Kikao Ikulu Chamwino Agosti 10, 2024.
Kikao hicho kilitoa dira na muelekeo chanya kwa Sekta ya Ushirika kuendelea kuhudumia Wanaushirika ili waweze kuzalisha zaidi na kukuza Uchumi na pato la Taifa.

Sekta ya Ushirika imepata msukumo wa kipekee katika Awamu ya Sita miongoni mwa mengi yanayoendelea kuimarisha Ushirika ni pamoja na Serikali kuchangia Mtaji wa Benki ya Ushirika kwa kiasi cha Billioni 5 zilizokuwa zikihitajika ili kuanzisha Benki hiyo. Tunatoa shukrani za kipekee kwa Mhe. Rais pamoja na Watendaji wa Serikali kufanikisha uanzishwaji wa benki hii.

Nitoe rai kwa Wanaushirika kutumia huduma zitakazokuwa zikitolewa na Benki yetu ya Ushirika (CBT) ambayo mwaka huu imefanikiwa kufanya Mkutano wake Mkuu wa kwanza. Benki hii inatarajia kuingia katika Soko la hisa na kujiendesha kibiashara kwa manufaa ya Wanaushirika na Taifa kwa ujumla.

Aidha , Serikali katika kuimalisha usimamizi imeanzisha mfumo wa kidijiatli wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) unaosimamiwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika ambao unaolenga kuimarisha usimamizi, kuongeza uwazi na weledi wa uendeshaji wa Vyama vya Ushirika kuanzia ngazi ya Wilaya hadi Taifa.

Tume katika jitihada za kuongeza Uwazi wa taarifa na kupunguza mianya ya ubadhirifu wa mazao ya Wakulima katika Vyama vya Ushirika imeunganisha Mfumo wa MUVU na Mizani za kidijitali. Mkulima anapokusanya mazao yake katika Chama cha Ushirika (AMCOS) hupima mazao kupitia Mizani hizo ambapo taarifa za mazao yake huingia kwenye Mfumo na kuonekana katika ngazi za Ushirika Wilaya, Mkoa na Taifa. Jambo ambalo limeongeza Uwazi na utunzaji Bora wa kumbukumbu na malipo stahiki kwa Wakulima.

Aidha, TCDC ipo katika hatua ya maboresho ya Kanuni za Vyama vya Ushirika za Mwaka 2015, kwa lengo la kuimarisha udhibiti na uhamasishaji wa Vyama vya Ushirika nchini.

Kwa kutambua mchango wa wanaushirika na wadau katika kukuza na kuboresha Sekta ya Ushirika nchini, TCDC inawaalika kuwasilisha maoni kwenye maeneo ambayo yanahitaji kufanyiwa maboresho/marekebisho kwenye Kanuni za Vyama vya Ushirika za Mwaka 2015.

Ninawashukuru Wanaushirika na Watanzania wote kwa kuendelea kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) kufanikisha dhamira yake ya kukuza na kuendeleza Ushirika ili uweze kuendeshwa Kibiashara kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi wa Vyama vya Ushirika nchini. Ushirikiano wa Tume na Wadau wa Ushirika umesaidia kupatikana kwa Mafanikio makubwa katika Sekta ya Ushirika.

"Ushirika- Pamoja Tujenge Uchumi"

# RAIS DKT. SAMIA AUNGA MKONO MAGEUZI KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akiongea katika Mkutano na Wanaushirika pamoja na Maafisa Ugani, Ikulu Chamwino, Agosti 2024.*

**RAIS** wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameunga mkono mageuzi yanayofanyika katika Vyama vya Ushirika nchini ili kulinda maslahi ya Wanaushirika na kurudisha hadhi ya Ushirika.

Akizungumza na Wanaushirika na Maafisa Ugani katika mkutano uliofanyika katika Ikulu ya Chamwino, Jijini Dodoma Agosti 10, 2024, Rais Samia amesema Vyama vya Ushirika ndiyo chombo madhubuti kinacholeta Maendeleo kwa watu wengi na kuondoa matabaka.

"Wanaushirika mmeanza kufanya mabadiliko muhimu yanayohitajika, ninawapongeza na endeleeni kusimamia vema maslahi mapana ya Wanaushirika," amesema Mhe. Rais.

Aidha, Mhe.Rais amewapongeza Wanaushirika kwa kuamua kuchangishana na kuanzisha Benki ya Taifa ya Ushirika nchini, ambayo itakuwa ngao yao katika upatikanaji wa fedha za mitaji kwa Vyama na Wanaushirika.

"Serikali inawapongeza kwa uamuzi huu muhimu wa kuanzisha Benki yenu Wanaushirika; na tutawaongezea Shilingi Bilioni tano (5) katika mtaji wa kuanzisha Benki hii muhimu kwa Wanaushirika na Wananchi kwaujumla," amesema Mhe. Rais.

Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu, amewapongeza Maafisa Ugani na watumishi wa Wizara ya Kilimo kwa kufanikisha nchi kujitosheleza kwa chakula na kuwa na ziada.

## MATUKIO MBALIMBALI KWENYE MKUTANO WA RAIS NA WANAUSHIRIKA PAMOJA NA MAAFISA UGANI











# NUKUU ZA VIONGOZI KUHUSU USHIRIKA

*"Wanaushirika mmeanza kufanya mabadiliko muhimu yanayohitajika, ninawapongeza na endeleeni kusimamia vema maslahi mapana ya Wanaushirika," -*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,*

*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan*



*Makamu wa Rais, Mhe. Dkt. Phillip Mpango*

*"Serikali inaendelea kuhamasisha Wakulima, Wafugaji na Wavuvi wajiunge katika Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) vitakavyokuwa chanzo cha Mikopo kwaajili ya kuendeleza shughuli zao na kuimarisha Uwekezaji katika Kilimo, Ufugaji na Uvuvi lakini pia Viwanda vya kusindika mazao ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi"*

# SACCOS TUMIENI MIFUMO YA KIDIGITALI - NAIBU WAZIRI SILINDE




*Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. David Silinde, akiongea na Wanaushirika wakati wa Ufunguzi wa Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Ushirika wa Akiba na Mikopo Duniani, Jijini Mwanza.*

**NAIBU** Waziri wa Kilimo, Mhe. David Silinde ametoa wito kwa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) kuendelea kutumia mifumo ya Kidigitali mbalimbali iliyopo sokoni inayoendana na uwezo wa Kifedha wa SACCOS ikiwemo mfumo ulioandaliwa na unaondeshwa na Muungano wa SACCOS nchini (SCCULT).

Mhe Silinde ameeleza kuwa, Mfumo huu umeandaliwa kwa mazingira ambayo ni rafiki na unaoendana na mahitaji ya SACCOS Nchini na SCCULT itatimiza jukumu lake na itawasimamia vema kwenye suala hili.

Ameeleza hayo tarehe 21/10/2024 wakati wa ufunguzi wa Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa Ushirika wa Akiba na Mikopo Duniani, yanayofanyika jijini Mwanza yenye kauli mbiu "Ulimwengu Mmoja Kupitia Ushirika wa Kifedha"

Mheshimiwa Silinde ameeleza Matumizi ya TEHAMA ni lazima kama Vyama vinataka kuendelea kuwahudumia wanachama vema na kuhimili ushindani uliopo kwenye soko la fedha na muendelee kutumia mfumo wa MUVU katika uendeshaji na usimamizi wa shughuli za vyama

"Umefika wakati sasa kuacha kabisa kujiendesha kwa mazoea na kutumia makaratasi, nafahamu kumekuwepo na mazoea ya kupuuza kwa makusudi maelekezo na ushauri unaotolewa ili kukuza sekta na kuboresha utendaji wa SACCOS zenu" amesema Mhe. Silinde.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya SCULLT, Khajat Aziza Mshana, amesema Maadhimisho haya yanafanyika kwa mara ya 76 Ulimwenguni tangu kuanzishwa kwake na mara ya 15 kwa Tanzania na SACCOS zimekuwa na nguvu na ushawishi wa kuunganisha jamii kwa kutoa Huduma ambazo zinagusa na kubadilisha maisha ya wanachama na jamii kwa ujumla.

## MATUKIO MBALIMBALI KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA KIMATAIFA YA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO (SACCOS)










# TANECU YAANZA SAFARI YA KUWA NA USHIRIKA IMARA KWA KUJENGA KIWANDA



*Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe (Mb), pamoja na Wanaushirika wakizindua kiwanda cha kubangua Korosho Newala, Mkoani Mtwara*

**CHAMA** Kikuu cha Ushirika cha Tandahimba na Newala (TANECU Ltd). kimeanza safari ya kuwa na Ushirika imara kwa kujenga kiwanda cha kubangua korosho Newala, mkoani Mtwara kilichogharimu kiasi cha shilingi bilioni 3.4.

Kiwanda hicho kimezinduliwa rasmi na Mhe. Hussein Bashe (Mb), Waziri wa Kilimo, tarehe 1 Oktoba 2024 ambapo maelfu ya wakulima wameshuhudia kwa hamasa za uhakika wa soko la mavuno ya korosho zao.

Waziri Bashe amekipongeza Chama Kikuu cha Ushirika cha TANECU Ltd. kwa kuwa mfano mzuri wa kuonesha ushirika unaozidi kuwa imara kwa kuhakikisha uwekezaji huo wa kiwanda ni wa wakulima wenyewe.

“Nielekeze pia kijengwe kiwanda kingine kama hiki kuleTandahimba ili kiwe tayari wakati wa msimu wa mwaka ujao,” amesema Waziri Bashe.

Kiwanda cha TANECU kina uwezo wa kubangua tani 3,500 kwa mwaka. Mkakati ni kuwa na viwanda 20 vya Kubangua Korosho chini ya TANECU katika Mkoa wa Mtwara ambapo 10 vitajengwa Newala (tayari 1 kimezinduliwa); na 10 vitajengwa Tandahimba.




*Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe (Mb) pamoja na Wanaushirika wakizindua Kiwanda cha Kubangua Korosho Newala, Mkoani Mtwara*

## MATUKIO MBALIMBALI KWENYE UZINDUZI WA KIWANDA CHA TANECU











# RC HOMERA AWATAKA WANANCHI KUTUMIA HUDUMA RASMI ZA KIFEDHA




*Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Mhe. Juma Homera akizindua Taarifa ya Utendaji wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo ya mwaka 2023.*

**MKUU** wa Mkoa wa Mbeya, Mhe. Juma Homera, ametoa wito kwa Wananchi kutumia Huduma rasmi za Kifedha zilizosajiliwa na zenye kutambuliwa ili kuepuka usumbufu unaotokana na huduma za Mikopo yenye kuumiza Wananchi kiuchumi.

Hayo yamesemwa Jijini Mbeya Septemba 5, 2024 wakati wa Uzinduzi wa Taarifa ya Utendaji wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) kwa mwaka 2023 iliyoandaliwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika.

Amesema, huduma jumuishi za kifedha kwa Watanzania ni sehemu ya malengo ya Serikali ambapo Benki Kuu ya Tanzania kwa kushirikiana na wadau, wamekuwa wakisimamia.

"Naomba nitoe wito kwa SACCOS kuendelea kufungua milango zaidi kwa wananchi, na kwenda maeneo mbalimbali ambayo huduma za kifedha bado hazijafika vizuri ili kufikia lengo la Serikali la kuhakikisha kuwa Watanzania wote wanafikiwa na mifumo rasmi ya huduma za kifedha," amesema.

Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege, akiwasilisha Taarifa hiyo amebainisha kuwa miongoni mwa malengo ya Taarifa hiyo ni kuweka uwazi na taarifa juu ya utendaji wa SACCOS nchini kwa mwaka husika na kujua maeneo yenye changamoto ili kuboresha zaidi.

Ameongeza kuwa kwa mwaka 2023 SACCOS zilizoomba Leseni ni 1,215, zilizopata Leseni ni 884 na zilizokosa Leseni ni 331. Akibainisha kuwa idadi hiyo inadhihirisha kuwa uelewa wa uendeshaji wa SACCOS umeongezeka na kuwataka wale ambao bado hawajakidhi vigezo wakamilishe taratibu husika.

"Niwaelekeze Viongozi wa SACCOS kuendelea kutekeleza vyema matakwa ya Sheria, Kanuni na Miongozo inayotolewa na Ofisi kwa kufanya Mikutano Mikuu ya Mwaka na kuwasilisha Bajeti za SACCOS hizo mapema na muendele kufungua matawi na milango ya huduma kwa mujibu wa Sheria na mfahamu kosa la jinai kuendesha shughuli za matawi na milango ya huduma pasipo kuidhinishwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika" amesema Dkt. Ndiege.

## MATUKIO MBALIMBALI KATIKA UZINDUZI WA TAARIFA YA UTENDAJI SACCOS 2023













# JE WAJUA?

## 1.0 Ukaguzi wa Ndani (Internal Audit)

Ukaguzi huu hufanywa au kutekelezwa na Mkaguzi/ Wakaguzi wa Ndani ambao ni Waajiriwa wa Taasisi husika. Ukaguzi wa ndani ni shughuli huru, yenye lengo maalum la kutoa uhakiki na ushauri unaolenga kuongeza tija na kuboresha utendaji wa Taasisi kwa kuchambua na kuboresha usimamizi wa vihatarishi kuimarisha udhibiti wa ndani na utawala Bora.

Lengo ni kutathmini hali ya uendeshaji wa Taasisi na kuona inaendeshwa na kusimamiwa kwa mujibu wa Sheria inayosimamia Taasisi husika na kwa manufaa ya Wanahisa, wateja/ wadau na Serikali kwa ujumla. Wakaguzi wa ndani ni sehemu ya Menejimenti ya Taasisi.

## 2.0 Ukaguzi wa Nje (External Audit)

Ni Ukaguzi huru unaofanywa na Wakaguzi ambao huteuliwa na Wanahisa, Wateja/ Wadau wa Taasisi au Serikali, na kuingia Mkataba wa kuikagua Taasisi husika. Wakaguzi hawa hukagua Hesabu za Taasisi na kutoa maoni yao yanayoonyesha kama Hesabu za Taasisi zilizokaguliwa zinawakilisha hali halisi ya Taarifa ya Fedha. Maoni ya Mkaguzi wa nje yanaweza kuwa ni; Hati safi (Unmodified Opinion Report), Hati yenye Mashaka (Modified Opinion

## 3.0 Aina za Ukaguzi katika vyama vya Ushirika

3.1 Ukaguzi wa Mara kwa mara (Continuous Inspection);
3.2 Ukaguzi wa Dharura (Surprise Inspection);
3.3 Ukaguzi Maalum (Special Inspection);
3.4 Ukaguzi wa mwisho; na
3.5 Ukaguzi wa nje



# TCDC NA CBE ZADHAMIRIA KUTOA MAFUNZO YA KUENDESHA USHIRIKA KIBIASHARA

**MRAJIS** na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, amesema Tume imedhamiria kushirikiana na Wadau kukuza na kuendeleza Ushirika ili uweze kuendeshwa Kibiashara kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi wa Vyama vya Ushirika.

Mrajis amesema hayo wakati wa utiaji saini wa Randama ya Makubaliano (MoU) kati ya Tume na Chuo cha Biashara (CBE) Novemba 20, 2024 Jijini Dodoma. Akiongea katika kikao hicho Mrajis amebainisha kuwa kwa sasa moja ya Vipaumbele vya Tume ni pamoja na kuhakikisha kuwa Ushirika unajiendesha kibiashara ili kutoa faida na kuongeza manufaa kiuchumi kwa Wanaushirika na wadau wengine.

Kwa upande wake Mkuu wa Chuo cha Biashara, Prof. Edda Lwoga, amesema CBE iko tayari kushirikiana na Tume katika kufanya Tafiti mbalimbali za kutatua changamoto za Ushirika, kutoa mafunzo yatakayosaidia kuendesha vyama kibiashara pamoja na kutoa Ushauri wa Kitaalamu.






*Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Dkt. Benson Ndiege pamoja na Mkuu wa Chuo cha Biashara (CBE) Prof. Edda Lwoga wakionesha Randama za Makubaliano kati ya Taasisi hizo, Jijini Dodoma*

Pamoja na mambo mengine, TCDC na CBE pia zitashirikiana katika kuwapa fursa wanafunzi wa CBE kujifunza kwa vitendo ili kupata uzoefu wa kimasomo pamoja na kuchangia ujuzi katika kuongeza tija ya uendeshaji wa Vyama vya Ushirika.

Kikao hicho kimehudhuriwa na Viongozi mbalimbali wa Tume pamoja na Chuo cha Biashara.

# UJUE MWONGOZO WA UWEKEZAJI KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA

Katika kung`arisha uwekezaji katika vyama vya ushirika tume imeandaa mwongozo wa uwekezaji ktaika vyama vya Ushirika utakao saidia kuelekeza vyama taratibu na za kuzingatia kabla na baada ya uwekezaji

Vilevile, mwongozo huu unatoa mwelekeo kwa viongozi wa Vyama vya Ushirika hususani Kamati ya uwekezaji ya Chama cha Ushirika pamoja na wanachama katika shughuli zote za uwekezaji kwa lengo la kuongeza tija katika uwekezaji naUmuhimu wa kuwa na Mwongozo wa Uwekezaji

• Kujenga imani kwa wanachama juu ya mwenendo wa uwekezaji wa chama chao kwa kupata taarifa ya mwenendo wa shughuli za uwekezaji na hatua za ufuatiliaji;
• Kuisaidia Ofisi ya Mrajis kuimarisha Usimamizi wa shughuli za uwekezaji zinazofanywa na Vyama vya Ushirika; na
• Kuwasaidia wadau wa Ushirika kufahamu taratibu na mashirikiano ya kiuwekezaji baina yao na Vyama vya Ushirika.

Maeneo ya Uwekezaji Kwenye Vyama vya Ushirika
Uwekezaji katika Vyama vya Ushirika umegawanywa katika maeneo manne (4)
kutegemeana na aina ya uwekezaji husika. Maeneo ya uwekezaji, kwa mujibu wa
kifungu cha 74 (1) cha sheria ya vyama vya Ushirika Na 6 ya mwaka 2013, ni: -
(i) amana inayotoa riba kwenye taasisi ya kifedha ya ushirika, au taasisi
yoyote ya kifedha kama itakavyoidhinishwa na Tume
(ii) hisa za chama kingine chochote kilichosajiliwa;
(iii) hati fungani za serikali na dhamana nyingine; na
(iv) uwekezaji mwingine kama Mrajis, kwa amri iliyoidhinishwa na Tume
na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali, kutamka uwekezaji ulioidhinishwa kwa madhumuni ya kifungu hiki ikiwemo Viwanda, Majengo, Mashamba, mifugo na uvuvi, usafirishaji na maeneo mengineyo, kadri yatakavyoelekezwa na Mrajis.

Vyama ambavyo vimetafuta wawekezaji kwenye mashamba yao badala ya kuwekeza vyenyewe, gharama ya uwekezaji (kodi) isipungue shilingi laki mbili kwa mwaka.

Uwekezaji kwenye Vyama vya Ushirika vya Kifedha kwa mujibu wa ya. 50(2) ya kanuni za huduma ndogo za kifedha [The microfinance (Saving and Credit Cooperative Societies) regulations)] za mwaka 2019, Vyama vya Ushirika vya akiba na Mikopo vinaweza kuwekeza kwenye maeneo yafuatayo:

(i) Amana za mabenki na taasisi za fedha zinazotoa riba (Interest bearing deposits of Banks or financial institutions);
(ii) Dhamana za Serikali (Government securities);
(iii) Vyama vingine vya kifedha;
(iv) Rasilimali zisizozalisha (non-earning assets); na
(v) Kwenye maeneo mengine ya uwekezaji kama itakavyoidhinishwa na Benki Kuu na Mrajis wa Vyama vya Ushirika;

### 3 Vigezo vya Uwekezaji

Ili kuepusha hasara inayoweza kujitokeza kutokana na shughuli za uwekezaji katika Vyama vya Ushirika, vigezo vifuatavyo vinatakiwa kuzingatiwa:

(i) Usalama wa fedha (safety);
(ii) Faida inayotokana na uwekezaji (yield);
(iii) kutawanya rasilimali na vihatarishi (Diversification);
(iv) Mahitaji ya fedha (liquidity);
(v) Mahitaji ya jamii (social responsibility); na
(vi) Uwekezaji unaoongeza thamani ya mali, bidhaa/mazao yanayozalishwa na wanachama na hali ya madeni ya chama (Liability Profile).

Itaendelea Toleo lijalo

## USHIRIKA WA GHOMACOS UNAVYONEEMESHA MAISHA WILAYANI SERENGETI




**MBOGAMBOGA** na Matunda ni miongoni mwa bidhaa za Mazao ya Bustani yanayozalishwa, kukusanywa na kuuzwa kupitia Vyama vya Ushirika. Tume ya Maendeleo ya Ushirika katika kutekeleza jukumu la kusimamia na kuhamasisha Vyama vya Ushirika tayari imeratibu uhamasishaji wa Vyama vya Ushirika wa Mazao ya Bustani Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Iringa, Songwe, Mbeya na Njombe zoezi hili ni endelevu kulingana na upatikanaji wa Rasilimali na Mipango ya Maendeleo.

Mkoani Mara, Wilaya ya Serengeti- Mugumu, Chama cha Ushirika wa Wakulima Wadogo wa Mboga, Matunda, Nafaka na Ufugaji (GHOMACOS) ni Ushirika uliopo pembezoni mwa Hifadhi ya Serengeti Wanachama wa GHOMACOS ni wanaushirika

kutoka katika maeneo ya Bunda, Serengeti na Grumeti Chenye kituo cha kukusanyia Bidhaa za Mbogamboga na Matunda eneo liitwalo Nata.

Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika GHOMACOS Masumbuko Mambassa anaeleza GHOMACOS ni Ushirika wenye jumla ya Wanachama 76 wanaozalisha bidhaa mbalimbali za mbogamboga na matunda zikiwemo Nyanyachungu, Kabeji, biringanya, nyanya, zukini, vitunguu, Matikiti Maji, viungo pamoja na uzalishaji wa Mayai na nyama ya Ng'ombe.
Mwenyekiti anasema, Chama hicho cha Ushirika kiliona fursa iliyopo katika kukuza na kuendeleza Utalii wa Ndani kwa kukusanya bidhaa zao za Mbogamboga na Matunda kwa pamoja na kuyauza katika Hoteli ya Kitalii iliyopo Serengeti iitwayo Grumeti, jambo ambalo limewafanya Wanaushirika wa Chama hicho kuwa na Soko la Uhakika wakati wote kutokana na mahitaji ya Chakula ya Kampuni hiyo inayoondesha shughuli zake katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

"Ukubwa wa Mahitaji ya Soko hilo yasingeweza kutoshelezwa na Mkulima mmoja mmoja kutokana na hali ya uzalishaji ya Wakulima hao Wadogo ila kupitia Ushirika, Wakulima hukusanya kwa pamoja katika kituo cha ukusanyaji wa Mazao yao ili kukidhi mahitaji ya soko," anasema Mwenyekiti.

Mwakilishi wa Kampuni ya Grumeti Beatrice Philemon anasema Kampuni hiyo sambamba na Vitengo vyake vyote ikiwemo Sabora, Sabayaya, Mara River hupeleka Mahitaji yake ya Chakula GHOMACOS kwa Barua pepe kila wiki ambapo kupitia uratibu wa Karani wa Chama Wanachama hukutana na kugawana Mahitaji ya Oda zile kulingana na viwango vya uzalishaji na aina ya Kilimo anachofanya.

Aidha, Malipo husika ya Mkulima anabainisha hufanyiwa kazi na kulipwa moja kwa moja katika Akaunti ya Benki ya Mkulima ndani ya kipindi cha makubaliano kati ya Chama na Kampuni. Hivyo, kuwezesha Chama kupanga kupanga na kuratibu masuala ya Chama kwa wakati.



*Baadhi ya bustani ya Wanachama wa Chama cha Ushirika GHOMACOS.*

Aidha, Malipo husika ya Mkulima anabainisha hufanyiwa kazi na kulipwa moja kwa moja katika Akaunti ya Benki ya Mkulima ndani ya kipindi cha makubaliano kati ya Chama na Kampuni. Hivyo, kuwezesha Chama kupanga kupanga na kuratibu masuala ya Chama kwa wakati.

Mkulima Magreth Mathayo Mwanachama GHOMACOS anasema soko hilo limewasaidia kutokana na urahisi wa ukusanyaji na uuzaji wa Bidhaa za Mbogamboga ambazo awali alikuwa akiuza peke yake mitaani jambo ambalo amesema lilikuwa lina changamoto kwani wakati mwingine bidhaa hazinunuliwi zote bali hubaki na kuharibika, jambo lililokuwa likileta hasara kwa Mkulima.

"Kwakweli soko la Grumeti limenisaidia sana kwani hata bei tunazouzia hapa ni tofauti kabisa na bei za mtaani, bei zipo juu zinatupa faida zaidi na uhakika wa kuuza bidhaa zetu na pia kutuwezesha kupata kipato cha kufanya mambo ya msingi," anasema Magreth

## USHIRIKI WA TANZANIA KATIKA MKUTANO MKUU WA SHIRIKISHO LA VYAMA VYA USHIRIKA DUNIANI (ICA) 2024

**MKUTANO** Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika Duniani umezinduliwa New - Delhi India, ambapo Watanzania kutoka Vyama mbalimbali vya Ushirika na Viongozi wa Serikali wanashiriki Mkutano huo.

Ujumbe wa Tanzania katika Mkutano huo unaongozwa na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo (Ushirika na Umwagiliaji), Dkt. Suleiman Serera, na Mrajis wa Vyama vya Ushirika Tanzania Bara, Dkt. Benson Ndiege..

Wadau wengine wanaoshiriki Mkutano huo ni pamoja na COASCO, MoCU, SCCULT, Bodi za Mazao, Vyama vya Mazao, Vyama vya Kifedha na Vyama vingine vya Ushirika.











## IMARISHENI MIFUMO KUZUIA UPOTEVU WA FEDHA KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA NAIBU KATIBU MKUU, KILIMO


*Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege, akitoa Taarifa ya Utekelezaji kwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Dkt. Stephen Nindi (kulia), alipotembelea TCDC*

**NAIBU** Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo – Ushirika na Umwagiliaji, Dkt. Stephen Nindi, ameiagiza Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) kuendelea kuimarisha na kuunda mifumo mbalimbali ya Kidigitali ili kudhibiti upotevu katika Vyama vya Ushirika na kuwahakikishia wanaushirika usalama wa fedha zao hasa wanapofanya mauzo ya mazao yao.

Ametoa agizo hilo Desemba 19, 2024 alipoitembelea TCDC kwa lengo la kujitambulisha, kujifunza na kusikiliza changamoto mbalimbali zinazoikabili pia kuskiliza maoni ya namna ya kutatua changamoto hizo.

Amesema kumekuwa na njia mbalimbali za ubadhilifu wa fedha za wanaushirika hasa kwa kutoa takwimu zisizo sahihi na ujanja mwingi ambao unapelekea ushirika kuonekana sio sehemu sahihi ya uwekezaji na kukwamisha maendeleo ya Ushirika, hivyo mifumo itasadia kukomesha ubadhilifu na kuongeza mapato ya serikali.

"Kuna baadhi ya mikoa wamekuwa wakitoa takwimu zisizo sahihi za wanachama, hasa wakati wa ugawaji wa pembejeo za kilimo na ujanja mwingi na ukwepeshaji wa fedha za serikali,. hivyo natoa agizo iundwe mifumo ya kuwahakikishia wanachama wa vyama vya ushirika usalama wa fedha zao," amesema Dkt. Nindi

Aidha, aliisisitiza Tume kuandaa na kushiriki kwenye makongamano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa kwa lengo la kujifunza mambo mbalimbali kuhusu ushirika ili kuboresha uendeshaji wa vyama hivyo kwa maslahi mapama ya Taifa.

Vilevile Dkt. Nindi, ameipongeza TCDC kwa hatua mbalimbali zilizochukuliwa kuhakikisha Ushirika unaaminika tena na wananchi ikiwemo kuanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Vyama Vya Ushirika (MUVU) na upimaji wa mazao ka kutumia Mizani ya Kidijitali na kuahidi kutoa ushirikiano wa kutosha kuhakikisha wanafikia malengo ya Serikali.

Naye, Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege, ameishukuru Serikali katika kuboresha na kuimarisha Ushiirika Nchini na amesema TCDC itaendelea kutekeleza maagizo yaliotolewa serikali kwa lengo la kuimarisha Ushirika.

**MATUKIO MBALIMBALI KATIKA CHA NAIBU KATIBU MKUU NA TCDC**














## MRAJIS ATEUA WAJUMBE WA BODI YA MPITO YA SHIRIKISHO LA VYAMA VYA USHIRIKA TANZANIA (TFC)



*Tito Haule, Mwenyekiti wa Bodi ya Mpito ya TFC*

**MRAJIS** na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, ameteua Wajumbe wa Bodi ya Mpito ya Shirikisho la Vyama Vya Ushirika Tanzania Bara (TFC) kwa mamlaka aliyonayo chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013.

Wajumbe walioteuliwa ni: Tito Haule (Mhadhiri, Taasisi ya Uhasibu Tanzania - TIA), atakuwa Mwenyekiti; Prof. Isaack Kazungu (Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi - MoCU); Wakili Shani Mayosa (Mkurugenzi, Huduma za Sheria - TIC); Tuse Joune (Mkurugenzi Mtendaji, Tanzania Bankers Association); Justica Masinde (Makamu Mwenyekiti, Bandarini SACCOS Ltd); Meja Michael Moyo (Mjumbe, Bodi ya Ngome SACCOS Ltd); Karimu Chipola (Mwenyekiti, Chama Kikuu cha Ushirika Tandahimba na Newala -TANECU Ltd); Shedrack Issangya (Mwenyekiti, Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Arusha); na Eliwaza Mkilya (Mjumbe, Bodi ya Mwenge Housing Cooperative Society Ltd).

Dkt. Ndiege amesema uteuzi huo umezingatia elimu, weledi, uzoefu, jinsia, na kaliba za wahusika; ikiwemo watu wa kutaka matokeo chanya ambao wanaweza kuifikisha TFC kwenye Maendeleo yanayohitajika.

Mrajis ameitaka Bodi hiyo ya Mpito baada ya makabidhiano na Bodi iliyomaliza muda wake kufanya tathmini ya Watendaji waliopo TFC kama wanaleta tija kwa Shirikisho, na utendaji wao unakidhi mahitaji na malengo ya Shirikisho ya wakati uliopo.

Aidha, Dkt. Ndiege amesema Ofisi ya Mrajis ipo tayari kushirikiana na Bodi ya TFC kutafuta Mtendaji Mkuu wa Shirikisho kama ilivyofanya katika Vyama Vikuu vya NCU LTD, SIMCU LTD na KNCU LTD.

Pia ameelekeza Bodi mpya kufanyia kazi Hoja za Mkaguzi wa Nje (COASCO) na Kuweka Mkakati thabiti wa kusimamia Shirikisho kwa Kuandaa Mpango Mkakati utakaoendana na wakati wa sasa, utakaotumika kama malengo mahsusi ya Shirikisho.



*Makao Makuu ya Shirikisho la Vyama Vya Ushirika Tanzania TFC, (USHIRIKA TOWER)*

## TCDC KUENDELEA KUWAJENGEA UWEZO WATUMISHI




*Mrajis na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dkt. Benson Ndiege akizungumza na Watumishi*

**MRAJIS** na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, amesema Tume itaendelea kuwajengea uwezo Watumishi katika utendaji na utekelezaji wa Majukumu yao ili kuongeza Ufanisi wa kazi kwa lengo la kuimarisha Sekta ya Ushirika.

Amesema hayo wakati akitoa Taarifa yake kwa Watumishi wa Tume wakati wa Kikao cha Watumishi Wote wa Tume Makao Makuu na Mikoani kilichofanyika Desemba 18, 2024 Jijini Dodoma.
Amebainisha kuwa Tume hufanya Vikao vya watumishi wote kila mwaka kwa lengo la kujadili kwa pamoja fursa na namna bora ya kutatua changamoto zinazojitokeza katika utendaji.

Amesema Tume tayari imekuwa na utaratibu wa kupeleka Watumishi wake katika Mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika Ngazi mbalimbali za masomo na kutenga fedha pamoja na Mpango wa mafunzo kwa Watumishi.

"Nitoe rai kwa Watumishi kutumia fursa za kujiendeleza hasa kitaaluma ili kujiongezea maarifa mapya kwaajili ya kujenga Ushirika imara," amesisitiza Mrajis.

Aidha, amesisitiza matumizi ya Mifumo ya TEHAMA ya kiutendaji kama vile Mfumo wa Upimaji wa Utendaji (e- Utendaji) ambao husaidia katika kufanya tathmini
ya utendaji wa majukumu ya Watumishi na Taasisi kwa ujumla, jambo linalosaidia kujua hali ya utendaji wa Taasisi ili kujua namna bora ya kuongoza na kusimamia huduma Bora za Ushirika.



Naye Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu Wizara ya Kilimo, Agnes Hugo, ameipongeza Tume kwa jitihada za kuendeleza na kujali Maslahi ya Watumishi kwa kuzingatia masuala yenye kuongeza Motisha na morali ya Kazi kwa Watumishi wa Tume. Watumishi wa Tume wameishukuru Tume kwa kuendelea kuboresha Mazingira ya Kazi na maslahi ikiwemo Mafunzo ya kuwajengea Uwezo, Michezo, maboresho ya Muundo pamoja na masuala ya Kijamii.

Kikao hicho kimejumuisha Watumishi wote katika Mikoa na Wilaya mbalimbali kwa njia ya Mtandao.

# VYAMA VYA USHIRIKA VYATEKELEZA MSINGI WA SABA WA USHIRIKA WA KUJALI JAMII


















# VIBONZO VYA USHIRIKA












MATANGAZO MBALIMBALI












# USHIRIKA NI FURSA




*Limetolewa na*

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)

Mtaa wa Kuu, S. L. P. 201, DODOMA.

Simu: +255 26 23 22456, Telefax: +255 26 23 21973

Barua Pepe: ushirika@ushirika.go.tz Tovuti: www.ushirika.go.tz

ushirika_tcdc

Tume ya Maendeleo ya Ushirika